



# ZIJUE HAKI ZAKO



KIJITABU KWA AJILI  
YA WAFANYAKAZI  
WA NDANI  
NCHINI QATAR

Kijitabu hiki kinaangazia haki kadhaa za msingi kama zilivyowekwa na Sheria za Uhamiaji na Wafanyakazi wa Ndani za Qatar.

**Kuna sheria za nyongeza.**

Kwa maswali yoyote, wafanyakazi wanatakiwa kwenda kwenye Wizara ya Maendeleo ya Utawala, Kazi na Mambo ya Jamii (wakiwa na nyaraka zote za ajira).

# MAMBO YENYEWE



**ZIJUE HAKI ZAKO**

# **MAZINGIRA YAKO YA KUISHI**

## MALAZI YAKO

### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 7 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

Mwajiri atakuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo:

- + Kutoa makazi mazuri kwa mfanyakazi wa ndani.

### HAKI ZAKO

---

- + Una haki ya kupata malazi ya kufaa, yaani yenye nafasi ya kutosha kitanda na kabati pasipo kujibana. Hii ina maana pia kwamba malazi yako ni safi na salama.
- + Na endapo unashirikiana chumba na mtu mwingine, basi ni lazima pawe na kitanda chako, falagha na usalama wa kutosha kwako na mali zako.



## AFYA YAKO

### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 7 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

Mwajiri atakuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo:

- + Kutoa huduma za matibabu, dawa na vifaa vya matibabu vinavyofaa pale unapotokea ugonjwa au kuumia wakati anatimiza wajibu wake, au litokanalo na hilo, pasipo kumtwisha mfanyakazi wa ndani mzigo wowote wa kifedha.

### HAKI ZAKO

---

- + Kama unajisikia vibaya au una hali ya afya ambayo inahitaji uangalizi wa kitibabu wa mara kwa mara, ni lazima umjulishe mwajiri wako na utembelee kituo cha afya haraka.



- + Nchini Qatar, unaweza kupiga 999 wakati wa dharula.
- + Una haki ya kumiliki na kuwa na kadi ya afya inayolipiwa na mwajiri kama sehemu ya mali zako.
- + Una haki ya kupata matibabu na kumwona daktari.

## CHAKULA CHAKO

### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 7 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

Mwajiri atakuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo:

- + Kutoa chakula cha kufaa kwa mfanyakazi wa ndani

### HAKI ZAKO

---

- + Una haki ya kupata chakula cha kutosha kujenga na kulinda afya yako.
- + Una haki ya kupata milo mitatu kwa siku bila malipo.



ZIJUE HAKI ZAKO

# MAHALI NA ASILI YA KAZI YAKO

## MAHALI PAKO PA KAZI



### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 9 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Mwajiri atazuiliwa kumwajiri mfanyakazi wa ndani nje ya Qatar, bila idhini ya mfanyakazi.

### HAKI ZAKO

---

- + Kama mwajiri wako anakutaka ukafanye kazi nje ya Qatar, una haki ya kukataa.
- + Mwajiri hana haki ya kukulazimisha kufanya kazi nje ya Qatar.

## MASAA YAKO YA KAZI



### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 12 CHA SHERIA NA. 15 YA MWAKA 2017

Mwajiri takuwa na wajibu wa kufanya yafuatayo.

- + Kiwango cha juu cha masaa ya kazi hakitazidi masaa kumi kwa siku, yakikatizwa na vipindi vya sala, mapumziko na chakula. Vipindi hivyo havitajumuishwa katika ukokotoaji wa masaa yaka kazi.

### HAKI ZAKO

---

- + Masaa yako ya kazi hayapaswi kuzidi masaa 10 kwa siku.
- + Mwajiri hana haki ya kukutaka ufanye kazi zaidi ya masaa 10 kwa siku. Mkataba wa kawaida wa mfanyakazi wa ndani unataja kwamba masaa ya kazi kwa siku ni masaa 8 pamoja na uwezekano wa masaa 2 ya nyongeza ya muda wa ziada. Kama unakubali kufanya kazi katika muda wa ziada, ilimradi masaa yanayotumika kufanyakazi kwa siku hayazidi masaa 10, basi mwajiri huyo lazima akulipe zaidi. Hii inapaswa kuwa sawa na mshahara wa msingi kwa masaa ya kazi ya
- + kawaida pamoja na malipo ya ziada yasiyopungua 25% ya mshahara wa msingi [mf. QAR 10 za mshahara wa msingi kwa saa + QAR 2.5 = Jumla yote kwa saa 1 ya muda wa ziada katika siku ya kazi ingekuwa QAR 12.5].



## LIKIZO YAKO YA MWAKA

### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 14 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Mfanyakazi wa ndani atakuwa na haki ya kupata likizo ya mwaka yenye malipo ya wiki tatu kwa kila mwaka uliotumika katika utumishi. Mfanyakazi anaweza kuigawa likizo hiyo, kuchagua muda na mahali ambapo itachukuliwa, isipokuwa kama kuna makubaliano kwenye mkataba.



### HAKI ZAKO

---

Una haki ya kupata likizo ya mwaka ya wiki tatu mwishoni mwa kila mwaka wa utumishi.

- + Una haki ya kuzihamishia kwenye mwaka unaofuata siku zozote za likizo zilizosalia ambazo hukuzitumia

## USALAMA WAKO

### SHERIA

---


#### KIFUNGU CHA 14 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Mfanyakazi wa ndani hatafanya kazi wakati wa likizo yake ya ugonjwa

### HAKI ZAKO

---

- + Una haki ya kupumzika na kutofanya kazi wakati wa ugonjwa. Mwajiri hawezi kukutaka ufanyakazi wakati wa ugonjwa.
- + Kulingana na mkataba wa kawaida wa wafanyakazi wa ndani, una haki ya kupata likizo ya ugonjwa yenye malipo ya wiki mbili kwa kila mwaka ambao umefanyakazi, baada ya kumaliza miezi mitatu ya kwanza ya kazi, ilimradi tu una cheti kutoka kwa daktari.



## MAPUMZIKO YAKO NA VIPINDI

### SHERIA

#### KIFUNGU CHA 14 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Mfanyakazi wa ndani hatafanya kazi wakati wa vipindi vyake vya mapumziko.

#### HAKI ZAKO (MAPUMZIKO NA VIPINDI)

- + Una haki ya kupumzika/vipindi vya mapumziko wakati wa kazi. Vipindi hivi ni kwa ajili ya mitu, ibada na kupumzika

## SIKU YAKO YA MAPUMZIKO

### SHERIA

#### KIFUNGU CHA 14 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Mfanyakazi wa ndani atakuwa na haki ya kupata likizo ya mapumziko ya kila wiki, yenye malipo, ambayo haipungui masaa 24 mfululizo.
- + Muda wa mapumziko ya kila wiki utaamuliwa kwa misingi ya makubaliano kati ya pande zote mbili kama ilivyoonyeshwa kwenye mkataba wa ajira.

#### KIFUNGU CHA 7 CHA SHERIA NA. 15 YA MWAKA 2017

- + Mfanyakazi wa ndani hatafanya kazi wakati wa mapumziko yake ya kila wiki, isipokuwa kama kuna makubaliano ya awali kati ya pande zote mbili yanayotengua sheria hii.

#### HAKI ZAKO

- + Una haki ya kuchukua siku nzima ya mapumziko kwa wiki.



- + Siku ya mapumziko lazima ikubaliwe kabla hujasaini mkataba na ni lazima ijumuishwe katika mkataba wa kazi.
- + Siku nzima haipungui masaa 24 mfulizo – siku ya mapumziko huchukuliwa nzima, si nusu nusu.
- + Katika siku yako ya mapumziko una haki ya kupata mapumziko kamili mbali na kazi/wajibu, isipokuwa kama umekubali kufanya kazi katika siku hiyo kwa malipo ya muda wa ziada. Mara chache na kwa ombi, kama unakubali kufanya kazi wakati wa siku yako ya mapumziko, una haki ya kuchukua masaa 24 ya mapumziko katika siku nyingine. Kwa nyongeza, una haki ya kulipwa kiasi sawa na mshahara wa msingi wa masaa ya kawaida ya kazi pamoja na malipo ya ziada yasiyopungua 15 ya mshahara wa msingi [mf. QAR 10 za mshahara wa msingi kwa saa + QAR 15 = Jumla yote kwa saa 1 ya muda wa ziada katika siku ya kazi ingekuwa QAR 25].
- + Ni muhimu kumjulisha mwajiri wako unapoondoka nyumbani wakati wa siku yako ya mapumziko.

**ZIJUE HAKI ZAKO**

**HAKI ZAKO ZA  
KIFEDHA**

## MSHAHARA WAKO

### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 8 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017



- + Mwishoni mwa mwezi, Mwajiri atawajibika kulipa mshahara wa kila mwezi kwa Qatari Riyals ambazo alikubaliana na mfanyakazi wa ndani, au katika siku ya tatu ya mwezi unaofuata, kwa kuchelewa.

### HAKI ZAKO

---

- + Una haki ya kupokea mshahara ulioahidiwa kwenye mkataba wako. Mshahara wa msingi wa kima cha chini wa Qatar ni QAR 1,000, na kamwe usipokee chini ya kiasi hiki. Kunaweza pia kuwa na mshahara wa kima cha chini ambao nchi yako imekubaliana na Qatar, na huu lazima uandikwe kwenye mkataba wako.
- + Una haki ya kupokea mshahara wako mwishoni mwa mwezi au katika tarehe mliyokubaliana, kila mwezi.
- + Mshahara wako lazima uingizwe kwenye akaunti yako ya benki au ulipwe kwako kwa pesa taslimu. Kama ukipokea mshahara wako kwa pesa taslimu, lazima upewe risiti na kuisaini ukithibitisha mshahara uliopokea.

## ADA ZA UAJIRI NA GHARAMA ZINAZOHUSIANA

SHERIA

KIFUNGU CHA 8 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017



- + Mwajiri hata ruhusywa kutoza ada, gharama au kamisheni yoyote kutoka kwa mfanyakazi kama fidia ya mchakato wa kuajiri kutoka nje na nchi.

HAKI ZAKO (ADA YA UAJIRI)

- + Mwajiri wako au wakala wa uajiri hawezi kufanya makato yoyote kutoka kwenye mshahara wako kwa ajili ya gharama zozote zinazohusiana na kuajiriwa kwako, ikiwa ni pamoja na nauli za ndege, vipimo vya afya, gharama za viza na ada ya uajiri.

## NAULI YAKO YA NDEGE

SHERIA

KIFUNGU CHA 8 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017




- + Mfanyakazi wa ndani pia atakuwa na haki, kwa kila miaka miwili ya utumishi, ya kupata tikiti ya ndege ya kurudi nchini kwake au mahali anapoishi kwa ajili ya likizo.
- + Mfanyakazi wa ndani anapoondoka Qatar baada ya kumaliza mkataba wake wa ajira au anaondoka kabla ya kumaliza mkataba kutokana na kuvunja sheria au mkataba wa ajira na mwajiri, mfanyakazi ana haki ya kupata tikiti ya kurudi nchini kwake au mahali anapoishi.

HAKI ZAKO

- + Unahaki ya kupokea tikiti ya ndege ya kurudi kutoka kwa mwajiri wako unapomaliza miaka miwili ya utumishi. Mwajiri wako lazima alipe gharama yote ya tikiti ya ndege, na wewe hutarajiwi kulipa sehemu yoyote ya gharama hiyo.
- + Kulingana na mkataba wa kawaida wa mfanyakazi wa ndani, kama unaamua kusitisha mkataba kabla ya tarehe yake ya mwisho huku ukizingatia kipindi cha notisi (bila uvunjaji wowote wa sheria au mkataba wa ajira na mwajiri), mwajili lazima achangie angalau sehemu ya gharama ya tikiti yako ya kurudi ya ndege. Mwajiri wako atalipa sehemu ya tikiti hiyo kulingana na muda halisi uliofanyakazi kotoka kwenye muda wa mkataba wako.
- + Mfano: Mkataba wako ulikuwa halali kwa muda wa miaka 2 (au miezi 24). Wewe uliamua kuusitisha baada ya miezi 18 na kurudi nchini kwako. Tuseme gharama ya tikiti yako ni QAR 1,500. Ili kukokotoa kiasi ambacho angalau mwajiri wako atalipa,
- + Hebu kwanza tuganye 1,500 kwa 24 (jumla ya muda wa mkataba wako):  $1,500 / 24 = 62.5$
- + Kwakuwa ulifanya kazi kwa miezi 18, mwajiri wako atalipa angalau  $62.5 \times 18 = \text{QAR } 1,125$

# MAFAO YAKO YA MWISHO WA UTUMISHI



## SHERIA

---

### KIFUNGU CHA 15 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017


- + Mwajiri atawajibika kulipa mafao ya mwisho wa utumishi kwa mfanyakazi wa ndani ambaye amekuwa katika utumishi kwa mwaka mmoja, kulingana na tarehe inayofaa ya Sheria ya Wafanyakazi wa Ndani
- + m.y. Septemba 12 mwaka 2017, pamoja na haki nyingine zozote.
- + Fao hili la mwisho wa utumishi litaamuliwa kwa makubaliano kati ya pande zote mbili ilimradi litakuwa angalau mshahara wa wiki tatu kwa kila mwaka wa utumishi. Mfanyakazi wa ndani atakuwa na haki ya sehemu za mwaka zikizidishwa kwa muda aliokaa katika utumishi.

### HAKI ZAKO (MAFAO YAKO YA MWISHO WA UTUMISHI)

---

- + Kama umefanyakazi na mwajiri mmoja kwa zaidi ya mwaka, una haki ya kupokea fao la mwisho wa utumishi kutoka kwa mwajiri wako.
- + Fao la mwisho wa utumishi halipungui mshahara wako kamili wa wiki tatu na hukokotolewa kwa kila mwaka uliofanya kazi.

# FIDIA YA KUUMIA KWAKO KAZINI



## SHERIA

---

### KIFUNGU CHA 15 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

- + Kwa ajali yoyote itakayomkuta mfanyakazi akiwa kazini, fidia itatolewa kulingana na masharti yanayotolewa na Sheria ya Kazi iliyotajwa hapo juu.

### HAKI ZAKO

---

- \* Endapo umeumia ukiwa kazini, una haki ya kupata fidia ya kuumia kazini.



ZIJUE HAKI ZAKO

**HAKI ZAKO ZA  
JUMLA CHINI YA  
SHERIA YA WA-  
FANYAKAZI WA  
NDANI**

# MKATABA WA AJIRA

## SHERIA

### KIFUNGU CHA 3 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017



- + Mfanyakazi wa ndani hataweza kuajiriwa isipokuwa kwa njia ya mkataba wa kazi, ambao umeandikwa na kuidhinishwa na Idara ukiwa katika nakala tatu. Kila upande utakabidhiwa nakala moja na nakala ya tatu itahifadhiwa idarani.
- + Mkataba wa ajira utandikwa kwa Kiarabu. Tafsiri ya mkataba huo kwa lugha nyingine unaweza kuambatanishwa. Mkataba wa ajira utajumuisha masharti yanayohusiana na mahusiano ya kiajira kati ya pande zote mbili.

Utajumuisha hasa vipengele vifuatavyo:

1. Jina la mwajiri, utaifa na mahali anapoishi.
2. Jina la mfanyakazi wa ndani, utaifa na mahali anapoishi.
3. Tarehe ya ukomo wa mkataba.
4. Aina na asili ya kazi aliyopewa mfanyakazi wa ndani.
5. Tarehe ya kuanza kazi na kipindi cha majaribio.
6. Muda wa mkataba, masharti ya kuongeza na kusitisha mkataba.
7. Mshahara uliokubaliwa, namna na tarehe ya malipo yake.
8. Masharti au vipengere vyovyote vilivyoainishwa katika sheria hii.

## HAKI ZAKO

- + Mwajiri hana haki ya kukuajiri mpaka pale atakapo saina mkataba wa ajira na wewe. Mkataba huu wa ajira ni lazima ujumuishe maelezo yote yanayotakiwakishe

# KUSITISHA MKATABA WAKO



## SHERIA

---

### KABLA YA MWISHO WA KIPINDI CHA MAJARIBIO

#### IBARA YA 1 YA SHERIA NA. 18 YA MWAKA 2020

- + Kama mfanyakazi anataka kubadilisha kazi wakati wa kipindi chake cha majaribio, lazima ampe mwajiri wake wa sasa notisi ya mwezi mmoja kupitia mfumo wa kielektroniki wa Idara ya Maendeleo ya Usimamizi, Kazi na Mambo ya Jamii (ADLSA). Lazima mfanyakazi aendelee kufanya kazi wakati wa kipindi cha notisi. Mwajiri mpya lazima amlipe mwajiri wa sasa fidia ya sehemu ya ada ya uajiri na gharama ya tikiti ya ndege, kama zipo. Kiasi kinachotakiwa kulipwa hakitazidi malipo sawa na mshahara wa msingi wa miezi miwili wa mfanyakazi.
- + Kama mfanyakazi anataka kusitisha mkataba wake wa ajira na kuondoka Qatar, lazima ampe notisi mwajiri wake wa sasa kupitia mfumo wa ADLSA. Lazima aendelee kufanya kazi wakati wa kipindi cha notisi kilichokubaliwa na mwajiri. Hata hivyo, kipindi cha notisi hakipaswi kizudi miezi 2.

#### KABLA YA MWISHO WA KIPINDI CHA MAJARIBIO IBARA YA 1 YA SHERIA NA. 18 YA MWAKA 2020

---

- + Kama mfanyakazi anataka kubadilisha kazi baada ya kipindi chake cha majaribio, lazima ampe notisi mwajiri wake wa sasa kama ilivyoelekezwa hapa chini:
- + Katika miaka miwili ya kwanza ya ajira, kipindi cha notisi kitakuwa mwezi mmoja.
- + Baada ya miaka miwili ya kwanza ya ajira, kipindi cha notisi kitakuwa miezi miwili.
- + Notisi lazima itolewe kupitia mfumo wa kielektroniki wa ADLSA.

- + Mfanyakazi lazima aendelee kufanya kazi na mwajiri katika kipindi hiki cha noti, isipokuwa kama pande zote mbili zimekubaliana vinginevyo.
- + Sheria hii inamhusu pia mfanyakazi anayetaka kusitisha mkataba wake wa ajira na kuondoka Qatar.

#### **WAKATI WOWOTE KATIKA KIPINDI CHA MKATABA KIFUNGU CHA 17 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017**

---

Mfanyakazi anaweza kusitisha mkataba wa ajira kabla ya mwisho wa muda wa mkataba huo huku akilinda haki zake zote mpaka fao la mwisho wa utumishi katika kesi yoyote kati ya zifuatazo:

1. Kama mwajiri hajatimiza matakwa yaliyoelezwa kwenye masharti ya sheria hii au kwenye mkataba wa ajira.
2. Ikiwa mwajiri au mtu aliyepewa mamlaka na mwajiri amedanganya wakati wa kumaliza mkataba na mfanyakazi, kwa mujibu wa vigezo vya mkataba.
3. Kama mwajiri au mwanafamilia wake anamchokoza mfanyakazi na kupelekea madhara katika mwili au maisha ya mfanyakazi.
4. Katika tukio la hatari kubwa ambayo inatishia usalama au afya ya mfanyakazi, na kama mwajiri alijua hatari hiyo, na hakufikiria kuiepusha.

#### **HAKI ZAKO**

---

- + Una haki ya kusitisha mkataba wako kabla ya mwisho wa muda wa mkataba huo kama unataka kubadilisha kazi au kama unataka kuihama nchi hiyo.
- + Wafanyakazi hawahitaji tena kibali cha Kutokuwa na Pingamizi ili kubadilisha kazi nchini Qatar. Ili kujua zaidi kuhusu mchakato wa kubadilisha kazi tafadhali tembelea tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Utawala, kazi na Mambo ya Jamii.

- + Una haki ya kusitisha mkataba wakati wowote ndani ya muda wa mkataba huo, bila kutakiwa kutoa notisi yoyote katika kesi zifuatazo:
- + Kama mwajiri wako hatimizi baadhi ya matakwa au matakwa yote yaliyomo kwenye mkataba.
- + Kama mwajiri au wakala wa uajiri anakudanganya kuhusiana na vigezo vya mkataba.
- + Kama mwajiri au mwanafamilia wake anakuumiza kimwili.
- + Kama kuna hatari kubwa inayotishia maisha au afya yako katika eneo lako la kazi.
- + Una haki ya kusitisha mkataba wako kabla ya mwisho wa muda wa mkataba huo kama unataka kubadilisha kazi au kama unataka kuihama nchi hiyo.
- + Wafanyakazi hawahitaji tena kibali cha Kutokuwa na Pingamizi ili kubadilisha kazi nchini Qatar. Ili kujua zaidi kuhusu mchakato wa kubadilisha kazi tafadhali tembelea tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Utawala, Kazi na Mambo ya Jamii.
- + Una haki ya kusitisha mkataba wakati wowote ndani ya muda wa mkataba huo, bila kutakiwa kutoa notisi yoyote katika kesi zifuatazo:
- + Kama mwajiri wako hatimizi baadhi ya matakwa au matakwa yote yaliyomo kwenye mkataba.
- + Kama mwajiri au wakala wa uajiri anakudanganya kuhusiana na vigezo vya mkataba.
- + Kama mwajiri au mwanafamilia wake anakuumiza kimwili.
- + Kama kuna hatari kubwa inayotishia maisha au afya yako katika eneo lako la kazi.

# NYARAKA ZAKO ZA UTAMBULISHO

## SHERIA

---

### KIFUNGU CHA 8 CHA SHERIA NA. 21 YA 2015



- + Mwijiri atarudisha paspoti au hati ya kusafiria kwa mfanyakazi anayetoka nje ya nchi baada ya kumaliza hatua za kibali cha kazi au hatua za kukifanya upya isipokuwa kama mfanyakazi huyo wa kutoka nchi nyingine anaomba kwa maandishi kwamba mwajiri amtunzie nyaraka hizo.

## HAKI ZAKO

---

- \* Una haki ya kutunza paspoti yako na nyaraka nyingine zozote za kusafiria kama mali yako, isipokuwa pale tu mwajiri wako anapovihitaji kwa ajili ya kupata kibali cha kuishi nchini au kuirejesha upya paspoti yako.
- \* Mwijiri anayeshikilia kwa nguvu nyaraka za kusafiria za mfanyakazi anakiuka sheria na atakabiliwa na faini isiyozidi Qr. 25,000.

# KUONDOKA NCHINI QATAR



## SHERIA

---

### IBARA YA 2 YA WIZARA YA MAAMUZI YA NDANI NA. 95 YA MWAKA 2019

- + Wafanyakazi wa ndani watakuwa na haki ya kuondoka nchini kwa muda mfupi au kuondoka moja kwa moja wakati wa uhalali wa mikataba yao ya kazi. Mfanyakazi atamjulisha mwajiri juu ya nia yake angalau masaa 72 kabla.

## HAKI ZAKO

---


- + Huhitaji tena kibali cha kutoka ili kuondoka Qatar. Hata hivyo unapaswa kumjulisha mwajiri wako kuhusu mipango yako ya kuondoka nchini angalau masaa 72 kabla. Unaweza kufanya hivyo kwa mdomo au kwa maandishi.

**ZIJUE HAKI ZAKO**

**HAKI YAKO YA  
KUTODHURIKA  
KIMWILI NA  
KISAIKOLOJIA**



## KUTODHURIKA KIMWILI NA KISAIKOLOJIA



### SHERIA

---

#### KIFUNGU CHA 7 CHA SHERIA NA. 15 YA 2017

Mwajiri ana wajibu wa


- + Kuwatendea vema wafanyakazi wa ndani kwa namna ambayo italinda utu na ustawi wao.
- + Kuepuka kuihatarisha afya au maisha ya mfanyakazi wa ndani, kumdhuru kimwili au kimaadili kwa namna yoyote ile.

### SHERIA

---

- + Una haki ya kutendewa kwa adabu na heshima na mwairi pamoja na jamaa wa nyumba yake.

## HAKI YAKO YA KUTOSHIKILIWA NA YA KUTOTESWA



### SHERIA

---

#### IBARA YA 36 YA KATIBA YA QATAR

Mwajiri atakuwa na wajibu wa

- + Mfanyakazi atahakikishiwa uhuru binafsi, na hakuna mtu anayeweza kukamatwa, kushikiliwa, kupekuliwa wala kuuwekea mipaka uhuru wake wa ukazi na wa kutembea, isipokuwa chini ya masharti ya sheria. Pia, hakuna mtu atakaye ingizwa katika mateso au matendo yanayodhalilisha utu wake. Mateso yatachukuliwa kama kosa la jinai linalostahili adhabu ya kisheria.

## **HAKI ZAKO (HAKI YAKO YA KUTOSHIKILIWA NA KUTOTESWA)**

---

- + Mwajiri hana haki ya kukuwekea kizuizi cha nyumbani kwake kinguvu.
- + Mwajiri hana haki ya kukuingiza katika matendo yoyote yasiyo ya kibinadamu, kama vile kukunyima chakula, kukuweka kizuizini kwa nguvu, kukusababishia madhara ya kimwili au kijinsia.


ZIJUE HAKI ZAKO

**WAJIBU  
WAKO CHINI YA  
SHERIA YA WAFAN-  
YAKAZI WA NDANI**

# WAJIBU

## SHERIA

### KIFUNGU CHA 11, SHERIA NA. 15 YA 2017



Mfanyakazi wa ndani atatakiwa kufanya yafuatayo

- + Kuheshimu sheria, mila, desturi pamoja na kanuni za kidini na kimaadili za nchi ya Qatar.
- + Kufanya kwa usahihi na kwa uaminifu kazi uliyokubali kuifanya, pamoja na kazi nyingine yoyote uliyooombwa kuifanya.
- + Kutunza siri, pesa na mali za mwajiri, wanafamilia na wageni wa mwajiri, na kujiepusha na kuyavuruga mambo wanayopendelea.
- + Kufuata maelekezo ya mwajiri na ya wanafamilia wa mwajiri kwa namna njema, isipokuwa kama wanakiuka sheria au mkataba wako wa ajira, au wanahatarisha maisha yako, au pesa, maisha au pesa za wengine.
- + Kuvitunza vifaa ulivyopokea ili kufanya kazi yako, ukivitumia kwa matumizi yaliyokusudiwa, kulingana na asili ya matumizi, na kuvirudisha kwa mwajiri mwishoni mwa muda wa utumishi.
- + Jiepushe na kufanya kazi zenye malipo au zisizo na malipo kwa ajili ya watu wengine, kwa kukiuka sheria au kanuni zinazotumika katika nchi ya Qatar.
- + Watendee vizuri mwajiri na familia ya mwajiri pamoja na wakazi, na ujiepushe na kuwadhuru, na hasa watoto na wazee

Kama mwajiri wako hatimizi baadhi au haki zako zote, unaweza kufungua malalamiko katika Idara ya Mahusiano ya Kazi ya Wizara ya Maendeleo ya Utawala, Kazi na Mambo ya Jamii.

Ili kufungua malalamiko, Wizara ina huduma ya simu za msaada ya masaa 24 za kupokea malalamiko na maoni kutoka kwa wafanyakazi kwenye namba 40280661 na 16008. Malalamiko ya kikazi pia yanaweza kutolewa kwa njia ya ujumbe mfupi, SMS, kwenda 92727 kwa kuingiza namba 5 na halafu namba yako ya QID au namba ya visa. Malalamiko ya kikazi yanaweza pia kutumwa kwenye barua-pepe ya wizara: [info@adlsa.gov.qa](mailto:info@adlsa.gov.qa) Wafanyakazi wanaweza pia kutumia Jukwaa Lililounganishwa la Wizara kwa Malalamiko na Kufichua Maovu.

Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa ushirikiano na  
Migrant-Rights.org likisaidiwa na Shirika la Kazi Duniani.

